**HOTUBA YA MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA(MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA UZINDUZI WA BODI YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO TAREHE 25 NOVEMBA, 2022 KATIKA UKUMBI WA OFISI ZA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO, JENGO LA UTUMISHI, JIJINI DAR ES SALAAM**

---

***Dkt. Laurean Ndumbaro; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,***

***Dkt. Mussa Muhiddin Kissaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,***

***Wajumbe wa Bodi; Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao***

***Eng. Benedict Ndomba, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)***

***Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),***

***Wanahabari,***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……………………………..***

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya njema, kuweza kukutana siku ya leo hapa katika ukumbi wa mikutano Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao, jengo la Utumishi, Jijini Dar es salaam. Hakika siku hii ni muhimu kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Umma na Utawala Bora na Serikali kwa ujumla, hususan katika matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma. Aidha ninatoa shukrani zangu za dhati kwa mapokezi mazuri na heshima kubwa mlionipa ya kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii ya Uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Napenda pia nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwako wewe Mwenyekiti Dkt Mussa M. Kissaka pamoja na wajumbe wa Bodi wote kwa kuteuliwa kwenu kuwa wakurugenzi kwenye Taasisi hii yenye dhamana ya

kusimamia matumizi sahihi na salama ya TEHAMA Serikalini na katika taasisi za umma, hongera sana.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kwa kuzingatia weledi na uzoefu wenu katika fani mbalimbali ni matarajio yangu kuwa Wajumbe wote wa Bodi mtashirikiana kikamilifu na Wizara kuhakikisha kuwa TEHAMA inatumika katika kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma, kufanya zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu. Hii ni pamoja na kuhakikisha Serikali inapata tija kulingana na uwekezaji uliofanyika na unaoendelea kufanyika katika utejekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kwa heshima na taadhima napenda nichukue fursa hii kumpongeza Rais  wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mheshimwa Samia Suluhu Hassan kwa juhudi anazofanya

kuhakikisha matumizi ya TEHAMA, ndani ya Serikali na Nchini kwa ujumla, yanakua kupitia uwekezaji mkubwa unaofanyika kwa kutenga Bajeti ya Serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa usambazaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili wananchi kila sehemu waweze kufikika kwa urahisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa njia ya mtandao, hata kwa kutumia simu za Mkononi za aina ya chini kabisa.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kama mnavyofahamu, Bodi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao inaundwa kwa Mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao Sura Na. 273, Kifungu namba 7 na kuipa majukumu kupitia Kifungu namba 8.

Ni kwa muktadha huo, uteuzi wa Bodi hii umefanyika kwa kuzingatia Sheria na vigezo vingine vingi ikiwemo uadilifu na uzalendo wenu kwa Nchi yetu. Hivyo dhamana mliyopewa na Serikali ni kubwa, na kama nilivyotangulia kusema hapo awali, ni matarajio yangu kuwa mtafanya

kazi yenu kwa uadilifu na uweledi wa hali ya juu kwa maslahi mapana ya Nchi yetu kulingana na Sheria, kanuni na miongozo husika ili kuhakikisha kwamba Mamlaka ya Serikali Mtandao inakidhi matarajio ya wadau na kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile mtatoa ushauri wa namna bora ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini na kuibua mikakati ya kutatua changamoto zinazowakabili Wananchi zinazoweza kutatuliwa kupitia Serikali Mtandao.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Kwa kuzingatia hayo yote, napenda kuwakumbusha mambo machache ya kuzingatia katika kazi zenu kama ifuatavyo:

1. Bodi itambue majukumu yake na kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa, na Bodi ifanye kila linalowezekana kuwajengea uelewa wadau mbalimbali kuhusu dhana nzima ya Serikali

Mtandao na umuhimu wake katika ustawi wa Taifa.

2. Bodi ifanye kazi kwa uadilifu mkubwa ili kuwa mfano kwa wale mnao waongoza. Ili Bodi ifanye kazi zake vizuri ni muhimu kutambua mipaka yake na wajibu wake na itoe ushirikiano kwa Menejimenti katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbali mbali zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli zake kulingana na Mpango mkakati.

3. Katika utekelezaji wa majukumu yenu, mtakumbana na changamoto nyingi kutoka kwa wadau wenu mbalimbali. Wadau na wafanyakazi wa Mamlaka watawapima kulingana na namna mnavyozitafutia ufumbuzi changamoto hizo, ambazo Mamlaka imekuwa ikikabiliana nazo ambazo ni pamoja na:

    a. Uwepo wa Mifumo ambayo haijumuishi taratibu za utendaji kazi (business processes) kuanzia mwanzo hadi mwisho (end-to-end)

katika baadhi ya taasisi za umma, hivyo kusababisha taratibu nyingine kufanyika nje ya mfumo au kwa kutumia mifumo mingine isiyowasiliana.

**b.** Upungufu wa wataalamu waliobobea katika usanifu, ujenzi na uendeshaji wa mifumo na miundombinu pamoja na usalama wa TEHAMA katika Taasisi za Umma

**c.** Kuongezeka kwa matishio ya usalama wa Mtandao na mabadiliko ya haraka ya Teknolojia

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Aidha, Bodi hii inaanza kazi katika kipindi ambacho mahitaji ya Serikali Mtandao ni makubwa sana na azma ya Serikali ni kuwa na Serikali ya kidijitali, hivyo ni matarajio yangu kuwa mtashiriki kikamilifu katika kutoa ushauri na kutekeleza yale yote yatakayoiwezesha Serikali ya kidigitali kutokea.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

Nisingependa kusema mengi au kuwachosha kwa kurudia hatua na mafanikio ya iliyokuwa Wakala na hatimaye Mamlaka ya Serikali Mtandao, kwani sote tumesikia kinagaubaga baadhi ya mafanikio kama yalivyoainishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa ufupi katika hotuba yake. Hivyo, ninawiwa kutoa pongezi za dhati kwa Bodi, ,uongozi wa Mamlaka pamoja Watumishi wake wote kwa Kazi nzuri mnazozifanya, ambazo zimeiwezesha Serikali kuboresha utendaji kazi wake na utoaji wa huduma kwa umma, zikiwa zinapatikana kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu, pamoja na kuiwezesha Serikali kuongeza makusanyo na udhibiti wa mapato yake.

Kwa upande mwingine, pamoja na kutoa kongole kwa mafanikio yaliyopatikana, nimeisikiliza kwa umakini hotuba ya Mkurugenzi Mkuu hususani alipogusia suala la mikakati mliyonayo katika kuimarisha utoaji huduma na hasa ile ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili Mamlaka.

Niseme kwamba ni azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kuwa utendaji kazi wa Serikali na Taasisi zake unaimarishwa kwa lengo la kuongeza mchango wake katika Uchumi wa Taifa. Ninawaahidi kuwa Wizara itaendelea kutoa ushirikiano na kuhakikisha inatekeleza ipasvyo wajibu wake kwa muktadha mzima wa kuboresha ufanisi wa Mamlaka. Vilevile kwa kadri nafasi itavyoruhusu itakuwa vema kukaa pamoja kufanya tathmini ya utendaji wa malengo ya tuliyopewa na tuliyojiwekea.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,**

**Mabibi na Mabwana,**

Baada ya Kusema hayo Machache, ninayo heshima kubwa kutamka kwamba, **Bodi ya Wakurungezi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao imezinduliwa rasmi**.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza**